JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA ISHIRINI

## KIKAO CHA THELATHINI NA NANE

29 JUNI, 2015

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA ISHIRINI

### KIKAO CHA THELATHINI NA NANE – TAREHE 29 JUNI, 2015

## I. MASWALI:

### OFISI YA WAZIRI MKUU:

**269. MHESHIMIWA JOSEPHAT SINKAMBA KANDEGE (KALAMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Maji ni uhai na ni muhimu sana kwa jamii:-

(a) Serikali ina mpango gani wa kuwapa huduma ya maji safi na salama Wananchi wa Jimbo la Kalambo;

(b) Vijiji vya Mwambao wa Ziwa Tanganyika vina shida kubwa sana ya upatikanaji wa maji safi na salama; Je, Serikali ina mkakati gani wa makusudi wa kuondoa adha hiyo kwenye maeneo hayo.

**270. MHESHIMIWA MENDRAD LUTENGANO KIGOLA (MUFINDI KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Makao Makuu ya Wilaya ya Mufindi ambayo zamani yalikuwa Mufindi Kibaoni yamehamishiwa Mafinga Mjini ambapo kwa sasa Mafinga ina Halmashauri ya Mji na Makao Makuu yake yako Mafinga:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa kuna umuhimu wa kurudisha Makao Makuu ya Halmashauri hiyo katika Jimbo la Mufindi Kusini;

(b) Jimbo la Mufindi Kusini ni kubwa na lenye idadi kubwa ya watu, Je, ni kwanini Makao Makuu hayo ya Halmashauri ya Mufindi isijengwe Igowole, ambapo ni katikati ya Jimbo na Wilaya kwa ujumla.

**WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:**

**271. MHESHIMIWA RACHEL ROBERT MASHISHANGA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:- Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga imeingia Mkataba na Mwekezaji wa Kiwanda cha nguo cha DAHONG TEXTILE CO. LTD kilichopo kijiji cha Nhelegeni Kata ya Kizumbi ambapo lengo lilikuwa kutengeneza

nguo kwa ajili ya kuuza ndani na nje ya nchi; lakini kwa bahati mbaya kiwanda hicho kimekuwa kikitengeneza nyuzi tu nazo hupelekwa nje:-

Je, ni kwa nini kiwanda hicho hakitengenezi nguo kama mkataba unavyohitaji.

**WIZARA YA KAZI NA AJIRA:**

**272. MHESHIMIWA AMINA MOHAMED MWIDAU (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kazi na Ajira:- Tanzania imebarikiwa rasilimali nyingi ikiwemo Bahari ya Hindi lakini vijana wengi wanaoishi mwambao wa Bahari hiyo hawana ajira ya uhakika na kipato chao ni cha chini sana:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha vijana hao wanapata ajira za uhakika kwa kutumia rasilimali ya Bahari ya Hindi.

## WIZARA YA AFYA NA USTAWI WA JAMII:

### 273. MHESHIMIWA KAPT. JOHN ZEFANIA CHILIGATI (MANYONI MASHARIKI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii:- Tangu Sera ya Wazee ipitishwe mwaka 2005 hadi sasa haijatungiwa Sheria:-

Je, Serikali iko tayari kushirikisha Wizara ya Afya na TAMISEMI ili kuhakikisha Sheria hiyo inatungwa haraka iwezekanavyo kuwasaidia Wazee hao kupata huduma bora za afya na mafao ya pensheni.

### 274. MHESHIMIWA KIDAWA HAMID SALEH (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii:- Wapo wanawake wajawazito wanaotumia vileo vikali na kuvuta sigara, bangi na mirungi:-

Je, ni madhara gani ya kutumia vileo vikali, sigara, bangi na mirungi kwa mtoto aliye tumboni mwa mama.

## WIZARA YA NISHATI NA MADINI:

## 275. MHESHIMIWA MESHACK J. OPULUKWA (MEATU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:-

Je, ni lini umeme utawashwa katika Kata za Mwanjolo, Bukundi, Mwamalola, Imalaseko, Mwamanongo na Mwabuzo vilivyopo katika Jimbo la Meatu.

## 276. MHESHIMIWA GOSBERT BEGUMISA BLANDES (KARAGWE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:- Katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013 na 2013/2014 Serikali iliahidi kupeleka umeme Tarafa nzima ya Nyabiyonza na vijiji mbalimbali vikiwemo Ruhita, Rukale, Kigarama, Chanika, Nyarugando, Nyakahita, Chonyonyo, Mushabaiguru nk:-

(a) Je, ni lini Mradi huo utaanza kutekelezwa na kukamilika;

(b) Je, ni kwa nini umeme hauwashwi katika vijiji vya Nyabwegira, vitongoji vya Karehe, Kamuli, Bisheshe, Ihembe I na Ihembe II na Nyakayanja pamoja na kwamba umeme unapita vijiji hivyo.

## WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

**277. MHESHIMIWA DIANA MKUMBO CHILOLO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- IGP Said Mwema alipotembelea kwenye Kituo cha Polisi cha Shelui Mkoani Singida aliahidi kuchangia shilingi Milioni tano (5,000,000/=) kwa ajili ya ujenzi wa jengo la kutunzia silaha; lakini hadi leo ahadi hiyo haijatekelezwa:-

Je, ni lini ahadi hiyo itatekelezwa ili jengo hilo liweze kukamilika.

## WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:

**278. MHESHIMIWA MARYAM SALUM MSABAHA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:- Chuo cha Sanaa Bagamoyo ni chuo kinachotambulika ndani na nje ya nchi:-

Je, ni lini Serikali itakipatia studio ya kisasa kama ile ambayo Mheshimiwa Rais aliitoa kwa **THT** pamoja na vifaa vingine ili wasanii wetu hasa wa muziki wafanye kazi zao kwa utaalamu zaidi.

## II. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

***(Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge zima na Kusomwa Mara ya Tatu)***

Muswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Benki ya Posta Tanzania wa Mwaka 2015 *[The Tanzania Postal Bank (Repeal and Transitional Provisions) Bill, 2015].*

Muswada wa Sheria ya Masoko ya Bidhaa wa Mwaka 2015 *(The Commodity Exchanges Bill, 2015);*

**DODOMA**
**29 JUNI, 2015**

**DKT. T. D. KASHILILAH**
**KATIBU WA BUNGE**